

Utambulisho Wangu Mtandaoni

Tafadhali andika majibu yako kwa maswali yanayofuata kwenye nafasi iliyowekwa.



Je, unaona utakuwa wapi miaka michache kuanzia sasa? Je, unataka kuwa mtu wa aina gani? Je, ni kazi ya aina gani ambayo wewe mwenyewe unaona utakuwa ukifanya au ni kwa namna gani utakuwa ukitumia muda wako?



Kwa kuzingatia mustakabali wako, unafikiri utakuwa unapendea nini? Utakuwa na maslahi gani? Vipi kuhusu burudani?



Je, ni aina gani ya ujuzi na nyenzo ambazo unadhani utakuwa umepata wakati huo? Je, unadhani utafurahia au kujivunia zaidi mafanikio ya aina gani?



Ukifikiria kuhusu wewe ni nani/uko wapi sasa, je, unafikiri mambo unayofanya sasa mtandaoni (kwa mfano, jinsi unavyojieleza na kutoa maoni, watu na jumuiya unazolingiliana nazo, vitu mnavyopenda au kufurahia pamoja kwa pamoja, stadi unazostawisha) yataathiri aina ya mtu utakayependa kuwa/wapi utakapopenda kuwa katika siku zijazo za hivi karibuni? Kama ndiyo, kwa njia gani? Au kama siyo, kwa nini?

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.